# Prendre sur nous le nom de Jésus-Christ

Par Dale G. Renlund
*du Collège des douze apôtres*

# Kujichukulia Jina la Yesu Kristo

Na Mzee Dale G. Renlund
*Wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili*

Conférence générale d'octobre 2025

*Plus nous nous identifions à Jésus-Christ et nous souvenons de lui, plus nous voulons être comme lui.*

En 2018, à l'université d'Utah, une chaire professorale spéciale a été créée. Elle porte le nom de « Chaire présidentielle de chirurgie cardio-thoracique du Dr Russell M. Nelson et de Dantzel W. Nelson »,cardio, faisant référence au cœur etthoracique, au thorax. Elle honore le travail important du président Nelson en tant que chirurgien et le soutien qu'il a reçu de sa défunte femme, Dantzel. Cette chaire professorale a été financée par un fonds appelé à durer dans le temps. La personne sélectionnée pour une chaire de ce prestige reçoit une récompense, un complément de salaire et des fonds pour faire de la recherche.

Le premier chirurgien choisi comme titulaire de cette chaire professorale était le Dr Craig H. Selzman, un chirurgien cardiaque talentueux qui n'est pas membre de notre Église. Lors de la cérémonie d'attribution de la chaire au docteur Selzman, de nombreux invités étaient présents, notamment le président Nelson et son épouse, Wendy. Au cours de la réunion, le président Nelson a parlé avec modestie de sa carrière de pionnier dans la chirurgie.

Ensuite, le Dr Selzman a expliqué ce que l'obtention de cette chaire signifiait pour lui. Il a raconté que, quatre jours auparavant, après une longue journée en salle d'opération, il avait appris que l'un de ses patients devait retourner au bloc. Il était fatigué et déçu, sachant qu'il allait devoir passer une autre nuit à l'hôpital.

*Kadiri tunavyojitambua na kumkumbuka Yesu Kristo, ndivyo tunavyotaka zaidi kuwa kama Yeye.*

Mwaka 2018, Chuo Kikuu cha Utah, kilianzisha uprofesa wa heshima uitwao "Kiti cha Urais cha Dkt. Russell M. Nelson na Dantzel W. Nelson katika Upasuaji wa Moyo na Kifua (Cardiothoracic Surgery)"—cardio, ikimaanisha moyo, nathoracic, ikimaanisha kifua. Hii inaheshimisha kazi muhimu ya Rais Nelson kama daktari wa upasuaji wa moyo na msaada aliopewa na marehemu mke wake, Dantzel. Uprofesa huu ulilipiwa na mfuko ulio sanifiwa ili udumu katika siku zijazo.Mtu aliye chaguliwa kwa aina ya uprofesa huu maarufu anapokea kutambuliwa, msaada wa mshahara na fedha za utafiti.

Daktari wa kwanza wa upasuaji wa moyo aliye chaguliwa kushikilia uprofesa huu alikuwa Dk. Craig H. Selzman, daktari mwenye umahiri wa upasuaji wa moyo ambaye si muumini wa Kanisa letu. Katika sherehe ya kutunza uprofesa huu kwa Dkt. Selzman, wageni wengi muhimu walihudhuria, wakiwemo Rais Nelson na mke wake Dada Wendy W. Nelson. Wakati wa mkutano, Rais Nelson alizungumza kwa kiasi kuhusu taaluma yake ya uanzilishi wa upasuaji wa moyo.

Kisha Dkt. Selzman alishiriki kile kilichomaanisha kwake kuteuliwa katika uprofesa huu. Alieleza kwamba siku nne zilizopita, baada ya siku ndefu kwenye chumba cha upasuaji, aligundua kwamba mmoja wa wagonjwa wake alihitaji kurudi kwenye upasuaji. Dkt. Selzman alikuwa amechoka na mwenye kukata tamaa, akijua kuwa angetumia usiku mwingine pale hospitali.

Ce soir-là, le Dr Selzman a eu une conversation avec lui-même qui a changé sa vie. Il s'est dit : « Vendredi, on va m'octroyer une chaire professorale portant le nom du Dr Nelson. Le Dr Nelson était connu comme quelqu'un qui maîtrisait ses émotions, qui traitait tout le monde avec respect et qui ne s'emportait jamais. Maintenant que mon nom va être associé au sien, je dois essayer de lui ressembler davantage. » Le Dr Selzman était déjà un chirurgien très bienveillant. Cependant, il voulait devenir encore meilleur.

Auparavant, l'équipe chirurgicale du Dr Selzman savait probablement quand il était fatigué et frustré, car cela transparaissait dans sa façon de parler et le ton de sa voix. Mais ce soir-là, au bloc opératoire, le Dr Selzman a fait un effort conscient pour être particulièrement encourageant et compréhensif envers son équipe. Il a eu l'impression que cela a fait une différence et il a décidé de continuer d'essayer de ressembler davantage au Dr Nelson.

Cinq ans plus tard, le président Nelson a fait don de ses archives professionnelles à l'université d'Utah. Des dignitaires de l'université sont venus le remercier officiellement. À cette occasion, le Dr Selzman a de nouveau pris la parole. Se référant aux initiales du président Nelson, RMN, il a dit : « Un esprit 'RMN' règne désormais au service de chirurgie cardio-thoracique de l'université d'Utah. »

Lorsqu'il fait face à des contrariétés, le Dr Selzman a expliqué : « Je fais ce que nous enseignons à nos internes, c'est-à-dire que je me concentre, je passe à autre chose et je fais de mon mieux. Cet esprit vit en nous chaque jour. Nous donnons, à chaque membre du service et à chaque nouvel interne, un badge à accrocher sur sa blouse. En bas de ce badge, on peut lire les lettres 'RMN'. L'esprit RMN est le fondement de notre formation ; nous l'enseignons à tout le monde. » Le Dr Selzman a modifié son attitude et ses aspirations antérieures, parce que son nom était dorénavant lié à celui du président Nelson.

Cette série d'événements impliquant le Dr Selzmanm'a amené à me demander : « Comment ai-je changé depuis que mon nom est associé à celui de Jésus-Christ ? Ai-je adopté un esprit chrétien ? Ai-je réellement essayé de devenir meilleur et plus semblable au Christ ? »

Dans l'expérience du Dr Selzman, nous pouvons voir au moins cinq parallèles avec le processus que nous suivons pour prendre sur nous

Jioni hii, Dkt. Selzman alikuwa na maongezi-ya-kubadilisha maisha yeye mwenyewe. Wakati huo, alifikiria, "Siku ya Ijumaa, nitateuliwa kwenye uprofesa unaoitwa kwa jina la Dkt. Nelson. Daima alijulikana kama mtu aliyedhibiti hisia zake, alimtendea kila mtu kwa heshima, na kamwe hakuwa na hasira.Sasa kwamba jina langu litakuwa limeunganishwa na lake, nahitaji kujaribu kuwa zaidi kama yeye." Dkt. Selzman tayari alikuwa daktari wa upasuaji mahiri. Lakini alitaka kuwa hata bora zaidi.

Hapo awali, timu yake ya upasuaji inawezekana kuwa ilijua kuhusu uchovu wake na kukasirika kwake kwa sababu aliruhusu ionekane kupitia mtindo wake na sauti yake. Lakini katika chumba cha upasuaji usiku huo, Dkt. Selzman alifanya jitihada za kuwa mwangalifu sana ili kuwa mwenye msaada maalum na mwenye kuielewa timu yake. Alihisi kwamba ilileta tofauti na aliazimia kuendelea kujaribu kuwa zaidi kama Dkt. Nelson.

Miaka mitano baadaye, Rais Nelson alichangia nyaraka zake za kitaaluma kwa Chuo Kikuu cha Utah.Watu mashuhuri kutoka Chuoni walikuja kumshukuru rasmi Rais Nelson.Wakati wa tukio hili, Dkt. Selzman alizungumza tena. Akitaja herufi za Rais Nelson, RMN, alisema, "Kuna maadili ya jamii katika 'RMN' ambayo sasa yanaenea katika Idara ya Upasuaji wa Moyo na Kifua katika Chuo Kikuu cha Utah."

Katika hali za kukata tamaa, Dkt. Selzman alieleza, "ninafanya kile tunacho wafundisha wanafunzi wetu kufanya—fokasi, sahau, na fanya vyema kadiri unavyoweza. Maadili haya yanaishi ndani yetu kila siku. Tunawapa pini za kifuani kila mshiriki wa idara na kila mwanafunzi mpya. Chini ya pini kuna herufi hizi'RMN.' Maadili ya RMN ni ya msingi kwa mafunzo yetu; tunayafundisha kwa kila mtu. Dkt. Selzman alikuwa kwa makusudi ameboresha mtazamo wake na matarajio yake ya awali kwa sababu jina lake sasa lilikuwa limeunganishwa na lile la Rais Nelson.

Mfululizo huu wa matukio unao mhusisha Dkt. Selzmanulinifanya nijiulize, "Je, mimi nimebadilikaje tangu nimeunganisha jina langu na jina la Yesu Kristo? Je, nimechukua maadlil kama ya Kristo kama matokeo yake? Je, nimejaribu kwa dhati kuwa bora na kuwa zaidi kama Yeye?

Katika uzoefu wa Dkt. Selzman, tunaweza kuona angalau milingano mitano ya mchakato ambao tunajichukulia juu yetu jina la Yesu Kris-

le nom de Jésus-Christ. Ce processus commence par le baptême, mais il n'est complet que lorsque nous devenons plus purs et saints, et lui ressemblons davantage.

Le premier parallèle est l'identification. En recevant la chaire Nelson, le Dr Selzman a associé son nom à celui du président Nelson et a commencé à s'identifier à lui. Quand nous prenons sur nous le nom de Jésus-Christ, nous associons notre nom au sien. Nous nous identifions à lui. C'est avec joie que nous nous faisons appeler chrétiens. Nous reconnaissons le Sauveur et nous nous affirmons résolument comme siens.

Autre parallèle très proche de l'identification : le souvenir. Quand le Dr Selzman entre dans son bureau, son regard est attiré par le médaillon qu'il a reçu quand il a été nommé à la chaire Nelson. C'est un rappel quotidien de l'esprit « RMN ». Pour nous, c'est la Sainte-Cène qui, chaque semaine, nous aide à nous souvenir de Jésus-Christ tout au long de la semaine. Lorsque nous prenons la Sainte-Cène, nous le faisons en souvenir du prix qu'il a payé pour nous racheter. Nous faisons de nouveau alliance de nous souvenir de lui, nous reconnaissons sa grandeur et nous apprécions sa bonté. Nous reconnaissons sans cesse que ce n'est que dans et par sa grâce que nous sommes sauvés de la mort physique et spirituelle.

Nous souvenir signifie que nous suivons le conseil d'Alma, le prophète du Livre de Mormon. « Que toutes [nos] actions soient pour le Seigneur, et, en quelque lieu que [nous aillions], que ce soit dans le Seigneur ; […] que toutes [nos] pensées soient dirigées vers le Seigneur ; […] que les affections de [notre] cœur soient placées à jamais dans le Seigneur. » Même lorsque nous sommes affairés dans d'autres domaines, nous continuons de penser à lui, tout comme nous nous souvenons de notre nom, quel que soit ce sur quoi nous portons notre attention.

Le troisième parallèle est une des conséquences du fait de se souvenir de ce que le Sauveur a fait pour nous : c'est l'imitation. Le Dr Selzman a commencé à imiter le président Nelson et l'esprit RMN. Je crois que la conduite du président Nelson est simplement la manifestation de toute une vie de disciple de Jésus-Christ. Pour nous, plus nous nous identifions à Jésus-Christ et nous souvenons de lui, plus nous voulons lui ressembler. En tant que disciples du Christ, nous de-

to. Ingawa mchakato huo unaanza na ubatizo, haukamiliki hadi pale tutakapo kuwa wasafi na watakatifu zaidi na kuwa zaidi kama Yeye.

Mlingano wa Kwanza ni utambulisho. Uteuzi wa Dkt. Selzman kwenye uprofesa wa Nelson uliunganisha jina lake na la Rais Nelson, na Dkt. Selzman aliaanza kujitambulisha pamoja na Rais Nelson. Tunapojichukulia juu yetu wenyewe jina la Yesu Kristo, tunaunganisha jina letu pamoja na Lake. Tunajitambulisha Naye. Tunafurahia kujulikana kama Wakristo. Tunamtambua Mwokozi na bila aibu tunasimama ili kuhesabiwa kama walio Wake.

Jambo linalohusiana kwa karibu na utambulisho ni mlinganisho mwingine—ukumbusho. Wakati Dkt. Selzman anapoingia ofisini kwake, macho yake yanavutwa kwenye medali aliyopokea alipochaguliwa kwenye uprofesa wa Nelson. Medali hii inamkumbusha kila siku kuhusu maadili ya RMN. Kwetu sisi, kushiriki sakramenti kila wiki kunatusaidia kumkumbuka Yesu Kristo kwa wiki nzima. Tunaposhriki sakramenti, tunafanya hivyo katika ukumbusho wa thamani ya gharama ambayo Yeye alilipa ili kutukomboa sisi. Tunafanya agano upya ili kumkumbuka Yeye, kutambua ukuu Wake na kuthamini wema Wake. Tunatambua tena na tena kwamba ni kwa neema Yake pekee tunaokolewa kutokana na kifo cha kimwili na kiroho.

Ukumbusho inamaanisha kwamba tunafuata ushauri uliotolewa na nabii Alma wa Kitabu cha Mormoni. Tunaacha "vitendo [vyetu] vyote viwe kwa Bwana, na po pote [tuendako, tuache] iwe kwa Bwana; … [tuache] mawazo [yetu] yote yaelekezwe kwa Bwana; … [na tuache] mapenzi ya [mioyo yetu] yawe juu ya Bwana milele."Hata wakati tunapo jihusisha na mambo mengine, bado tunamkumbuka Yeye, kama tunavyo kumbuka majina yetu wenyewe, bila kujali kile kingine tunacho zingatia.

Ukuaji wa kukumbuka kile alichotufanyia Mwokozi ni mlingano wa tatu—kufuata mfano. Dkt. Selzman alianza kumuiga Rais Nelson na maadili ya RMN. Ninaamini kwamba maadili ya Rais Nelson ni dhihirisho tu la uanafunzi wake wa maisha yote kwa Yesu Kristo.Kwetu sisi, kadiri tunavyojitambua na kumkumbuka Yesu Kristo, ndivyo tunavyotaka kuwa zaidi kama Yeye. Kama wanafunzi wake, tunabadilika kuwa bora tunapo fokasi Kwake, zaidi ya tunapojitazama sisi

venons meilleurs quand nous nous concentrons sur lui, bien plus que lorsque nous nous concentrons sur nous-mêmes. Nous nous efforçons de devenir comme lui et nous cherchons à acquérir ses vertus. Nous prions ardemment afin d'être remplis de charité, l'amour pur du Christ.

wenyewe. Tunajaribu kuwa kama Yeye na kutafuta kubarikiwa kwa sifa Zake. Tunasali kwa bidii ili tujazwe na hisani, ule upendo msafi wa Kristo.

En avril, le président Nelson a enseigné : « Si la charité devient une part intégrante de notre caractère, nous perdrons l'envie de rabaisser autrui. Nous cesserons de juger. Nous serons charitables envers tous les hommes, quel que soit leur milieu. Éprouver de la charité pour tous […] est essentiel à notre progression. La charité est le fondement même d'une personnalité divine. » En parallèle de la charité, nous cherchons àcultiver […] et développerles autres dons spirituels du Sauveur, notamment l'intégrité, la patience et la diligence.

Kama Rais Nelson alivyofundisha mwezi Aprili: "Kadiri hisani inavyokuwa sehemu ya asili yetu, tutakosa hamu yaa kuwadhalilisha wengine. Tutaacha kuwahukumu wengine. Tutakuwa na hisani kwa wale wanaotoka katika hali zote za maisha. Hisani kwa watu wote … ni muhimu kwa ajili ya maendeleo yetu. Hisani ni msingi wa sifa ya uchamungu"Sambamba na hisani, tunatafuta,"kukuza, … na kupanua"zawadi nyingine za kiroho kutoka kwa Mwokozi, zikiwemo uadilifu, uvumilivu na bidii.

Le fait d'imiter Jésus-Christ nous amène au quatrième parallèle : conformer notre volonté à la sienne. Nous nous joignons à lui dans son œuvre. En tant que chirurgien, le Dr Nelson était un pédagogue, un soignant et un chercheur. Le badge sur les blouses utilisées dans le service du Dr Selzman met l'accent sur ces engagements en affichant les motsenseigner,soigneretdécouvrir. En ce qui nous concerne, le fait de prendre sur nous le nom de Jésus-Christ implique, entre autres, que nous conformions volontairement, intentionnellement et avec enthousiasme nos buts aux siens. Nous nous joignons à lui dans son œuvre quand nous « aimons, faisons connaître et invitons». Nous nous joignons à lui dans son œuvre quand nous servons nos semblables, surtout ceux qui ont été blessés, brisés ou écrasés par leurs expériences dans la condition mortelle.

Kumuiga Yesu Kristo kunatuongoza kwenye mlingano wa nne—mfungamano na madhumuni Yake. Tunaungana Naye katika kazi Yake. Kama daktari wa upasuaji, Dkt. Nelson alijulikana kama mwalimu, mponyaji na mtafiti. Pini kwenye mkunjo wa koti kifuani inayotumika katika Kitengo cha Dkt. Selzman inasisitiza kazi hizi, zikionyesha manenofundisha,ponya, nagundua. Kwetu sisi, sehemu ya kujichukulia juu yetu jina la Yesu Kristo inahusisha kwa hiari, kwa kukusudia, na kwa shauku kufungamanisha malengo yetu na Yake.Tunaungana Naye katika kazi Yake wakati "tunapopenda, tunaposhiriki na tunapoalika."Tunaungana Naye katika kazi Yake tunapowatumikia wengine, hasa wale walio katika hatari na wale ambao wamejeruhiwa, kuharibiwa au kupondwa na uzoefu wao wa duniani.

Nous prenons plus pleinement sur nous le nom de Jésus Christ lorsque nous nous identifions à lui, nous nous souvenons de lui, nous l'imitons et nous nous conformons à sa volonté. Ces quatre actions mènent à un cinquième parallèle : l'habilitation. Nous accédons au pouvoir de Dieu et à ses bénédictions dans notre vie. La chaire Nelson a permis au Dr Selzman de recevoir une reconnaissance et un fonds de soutien qu'il utilise pour changer la culture de son service. Il utilise cette « dotation de pouvoir » pour aider les autres. De la même manière, quand nous prenons sur nous le nom du Sauveur, notre Père céleste nous accorde son pouvoir pour nous aider à remplir notre mission dans la condition mortelle.

Kwa hiyo tunajichukulia juu yetu jina la Yesu Kristo kwa ukamilifu zaidi kupitia utambulisho, ukumbusho, kuiga mfano na mfungamano.Kutenda haya manne yanatuongoza kwenye mlingano wa tano—uwezeshaji. Tunafikia nguvu na baraka za Mungu katika maisha yetu. Uprofesa wa Nelson unampa Dkt. Selzman utambulisho na fedha za msaada ambazo anazitumia kubadilisha utamaduni katika idara yake. Yeye anatumia hii "baraka ya nguvu" ili kuwasaidia watu wengine. Kwa njia hiyo hiyo, tunapojichukulia sisi wenyewe jina la Mwokozi, Baba yetu wa Mbinguni anatubariki kwa nguvu zake ili kutusaidia kutimiza misioni yetu katika maisha ya duniani.

Lorsque nous contractons des alliances supplémentaires avec Dieu, nous prenons plus pleinement sur nous le nom de Jésus-Christ. En conséquence, Dieu nous bénit en nous accordant davantage de son pouvoir. Comme le président Nelson l'a enseigné : « Chaque personne qui contracte des alliances dans les fonts baptismaux et les temples, et qui les respecte, bénéficie d'un accèsplus grandau pouvoir de Jésus-Christ. […] Le respect des alliances avec Dieu apporte en récompense le pouvoir céleste, pouvoir qui nous fortifie pour [mieuxsurmonter] nos épreuves, [résister à] nos tentations et [affronter] nos chagrins. »

Nous devenonsplusréceptifs spirituellement. Nous avonsdavantagede courage pour affronter des circonstances impossibles en apparence. Nous sommesdavantagefortifiés dans notre détermination à suivre Jésus-Christ. Nous nous repentons et retournons à luiplusrapidement quand nous transgressons. Nous faisonsmieuxconnaître son Évangile par son pouvoir et son autorité. Nous aidons les personnes dans le besoin sans les juger. Nous les jugeons vraiment beaucoup moins. Nous conservons le pardon de nos péchés. Nous éprouvons une paix plus grande et nous sommes plus joyeux, parce que nous pouvons nous réjouir continuellement. Sa gloire nous entourera et ses anges nous garderont.

Voici l'invitation du Sauveur : « [Venez] au Père en mon nom et [recevez] sa plénitude en temps voulu. » Je vous exhorte à le faire. Venez à notre Père céleste, Prenez sur vous le nom de Jésus-Christ. Identifiez-vous à lui. Souvenez-vous toujours de lui. Efforcez-vous de lui ressembler. Joignez-vous à lui dans son œuvre. Recevez son pouvoir et ses bénédictions dans votre vie. Gravez son nom dans votre cœur, volontairement et intentionnellement. Ainsi, vous honorerez votre « position » devant Dieuet vous serez qualifiés pour que le Sauveur intercède en votre faveur. Vous deviendrez un héritier exalté dans le royaume de notre Père céleste, cohéritier du Premier-Né, notre Sauveur et Rédempteur bien-aimé.

Il vit. Je le sais de manière absolue. Il vous aime. Il a donné sa vie pour vous. Il vous supplie de venir au Père à travers lui. Au nom de Jésus-Christ. Amen.

Tunapofanya maagano ya ziada na Mungu, tunajichukulia juu yetu wenyewe kwa ukamilifu zaidi jina la Yesu Kristo.Kama matokeo yake, Mungu anatubariki zaidi kwa nguvu Zake. Kama Rais Nelson alivyofundisha: "Kila mtu anayefanya maagano katika visima vya ubatizo na hekaluni—na kuyashika—ameongezaufikiaji wa nguvu ya Yesu Kristo. … "Thawabu ya kushika maagano na Mungu ni nguvu ya mbinguni … ambayo inatuimarisha sisi ili kustahimili majaribu, vishawishi na maumivu yetu ya moyovyema zaidi."

Tunakuwa wapokeajizaidikiroho. Tunakuwa na ujasirizaidiwa kukabiliana na hali zisizowezekana. Tunaimarishwazaidikatika azma yetu ya kumfuata Yesu Kristo. Kwa harakazaiditunatubu na kurudi Kwake pale tunapovunja sheria. Tunakuwabora zaidikatika kushiriki injili Yake kwa nguvu Yake na mamlaka. Tunawasaidia wale walio katika shida bila ya kuwahukumu, bila kuwahukumu kabisa. Tunabakisha ondoleo la dhambi zetu. Tunakuwa na amani kubwa, na tunakuwa wenye shangwe zaidi kwa sababu daima tunaweza kushangilia.Utukufu wake utatuzunguka, na malaika Wake watakuwa na dhamana juu yetu.

Mwokozi anatualika, "Njooni kwa Baba katika jina langu, na katika wakati wake mtapokea utimilifu wake."Ninawasihi kutenda haya. Njooni kwa Baba Yetu wa Mbinguni. Jichukulie juu yako jina la Yesu Kristo. Jitambulishe pamoja Naye. Daima mkumbuke Yeye. Jitahidi kuwa kama Yeye. Jiunge Naye katika kazi Yake. Pokea nguvu na baraka Zake katika maisha yako.Andika jina Lake moyoni mwako, kwa hiari na kwa kusudia. Hii inakupa wewe "hadhi" mbele za Munguna kukustahilisha kwa ajili ya uombezi wa Mwokozi kwa niaba yako.Utakuwa mrithi aliyetukuka katika ufalme wa Baba yetu Mbinguni, mshirika wa urithi pamoja na Mzaliwa Wake wa Kwanza, Mwokozi wetu mpendwa na Mkombozi.

Yeye yu hai. Hakika ninajua hivyo. Yeye anakupenda. Yeye alitoa uhai Wake kwa ajili yako. Yeye anakusihi uje kwa Baba kupitia Kwake. Katika jina la Yesu Kristo, amina.